# TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM

## Hotuba ya Mkuu wa Taasisi ya DIT kwa Wanafunzi Wote

PROFESA PREKSEDIS MARCO NDOMBA

**MKUU WA TAASISI**

Imehaririwa na Bw. Iginas Mangula

**11 NOVEMBA 2016**

**HOTUBA YA MKUU WA TAASISI YA DIT, PROF. PREKSEDIS MARCO NDOMBA, KWA WANAFUNZI WOTE ILIYOTOLEWA SIKU YA IJUMAA, TAREHE 11 NOVEMBA 2016 KATIKA UKUMBI WA CHAKULA**

Naibu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu (DPARC); Prof. Christian Nyahumwa;Naibu Mkuu wa Chuo, Utawala na Fedha (DPAF); Dkt. Mashauri A. Kusekwa;Msajili wa wanafunzi,, Bw. Roy Elineema;Wakuu wa Idara za Kitaaluma na Utawala:Dkt. Anthony Thomas (Civil Engineering); Dkt. Dalton Kisanga (Computer Studies); Dkt. Sostenes Karugaba (Electrical Engineering); Dkt. Georgia Rugumira (Eletronics and Telecommunications Engineering); Dkt. Edwin Rutalebwa (General Studies); Dkt. Fredrick Sanga (Mechanical Engineering); Dkt. Patrick Nsimama (Laboratory Science and Technology); Dkt. John Msumba (Industrial Liaison Officer); Dkt. Joseph Matiko (Library Services); Dkt. Florence Mamboya (Research, Publications and Postgraduate Studies); Dkt. Leonia Henry (Examination Officer); Bw. Daudi Mboma (India-Tanzania Centre of Excellence of Information and Communication Technology: IT-CoEICT); Dkt Joseph Mkilania (Institute Consultancy Bureau: ICB); Dkt. Amos Nsanganzelu (Chief Internal Audit: CIA); Dkt. Respicious Kiiza (Coordinator Research, Publications and Postgraduate Studies); Dkt. Ezekiel Amri (Coordinator Curriculum); Dkt. Albert Mmari (Mwanza Campus); Bw. Ambogo Ambogo (Myunga Campus, Songwe); Bw. Raphael Nzumbi (Admission Officer); Bw. Joseph Challo (Quality Assurance Bureau); Bw. Venance Ngunga (Chief Accountant: Bursar); Bi. Zaibabu Mbwambo (Estates Manager); Bw. Haruna Mashebe (Procurement Management Unit); Bw. Ombeni Mnzava (Information Communication Technology); Bw.

Leonard Mduma (Planning office); Bw. Nelson Ndelwa (Legal Officer); Bw. Yosiah Misago (Dean of Students); Bw. Godwin Ndeki (Dispensary); Bw. Sebastian Inoshi (Human Resource and Administration); Bw. Amani Kakana (Public Relations Officer: PRO); Bi. Nsatusile Nzowa (RAAWU Chairperson); Bw. Chogo Chogo (RAAWU Secretary); Dkt. Daudi Simbeye (THTU Chairperson); Bw. Labani Singoye (THTU Secretary); Dkt. Salha Kassim (Academic Staff Association: ASA, Chairperson); and Dkt. Petro Pesha (Acting ASA Secretary); Rais wa Serikali ya Wanafunzi (DITSO), Bi. Zuhura Abdulrahaman, na mjumbe wa Bodi ya Taasisi; viongozi waandamizi wa serikali ya wanafunzi (DITSO); wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza OD, GC, BENG, MENG; wanafunzi wote wa mwaka wa pili; wanafunzi wote wa mwaka wa tatu;OD, BENG wanafunzi wote wa mwaka wa nne BENG; Mabibi na Mabwana. Habari za mchana!

**Ndugu wanafunzi,**

Kwanza kabisa napenda kukiri kwamba nimefarijika sana kupata fursa hii ya kukutana nanyi. Hotuba hii ambayo inaitwa "Chief Executive Officer (CEO) Speech" ni ya kipekee na ni ya nadra kwani hutolewa na Mkuu wa Taasisi Mpya kwa lengo la kujitambulisha rasmi, kuongelea maono na vipaumbele vya Taasisi. Pamoja na ukweli kwamba nilishaitoa hotuba inayofanana na hii kwa wafanyakazi wote wa DIT siku ya Alhamis, tarehe 4 Agosti 2016; bado ninaamini kwamba wanafunzi wanastahili kusikia na kuchangia kwa yale yote yaliyozungumzwa siku hiyo kwa mustakabali wa Taasisi. Aidha, mimi binafsi naamini kuwa wanafunzi ni nguzo imara ya taasisi ya elimu ya juu kama hii ya kwetu.

Kabla ya kuendelea na hotuba yangu napenda niwakaribisheni wote kwa ujumla wenu hapa Chuoni bila kujali ulishawahi kukaribishwa nami hapo awali. Kwa wale wanafunzi wa mwaka wa kwanza naamini bado mnakumbuka hotuba yangu ya ukaribisho niliyoitoa wiki iliyopita siku ya Ijumaa, tarehe 4 Novemba 2016 hapa hapa ndani ya Ukumbi wa Chakula (DH). Pamoja na ukweli kwamba niligusia baadhi ya maono na vipaumbele vya Chuo katika hotuba ile, lakini sikuweza kutoa msistizo stahiki kama nitavyofanya kwenye hotuba ya leo.

**Ndugu wanafunzi,**

Nadhani kwa wale wanafunzi waliokaa hapa Chuoni miaka miwili, mitatu, au minne watapenda kumjua huyu aliyesimama na kuongea mbele yenu. Mimi ni Mkuu mpya wa Taasisi ya DIT niliyeanza kufanya kazi rasmi hapa Chuoni kuanzia tarehe 1 Julai 2016, nikitokea Chuo cha Kampasi cha Uhandisi na Teknolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Mlimani); ambapo wengi wenu mnakisikia au kukifahamu vizuri sana. Kimsingi, nimekuja kushirikiana na wanajumuiya wa DIT wakiwemo wanafunzi, walimu na wafanyakazi waendeshaji katika kusukuma gurudumu la maendeleo la nchi hii hasa katika tasnia ya elimu ya ufundi. Aidha, napenda kuweka bayana kuwa nilifurahia sana kuja kuiongoza DIT kwani, licha ya kuwa ni taasisi ya elimu ya juu kongwe sana hapa nchini, iliyoanzishwa mwaka 1957, DIT imepata mafanikio makuwa sana kama vile kusomesha watu maarufu hapa nchini, baadhi yao wakiwemo Prof. Mathew Luhanga (Makamu Mkuu mstaafu wa Chuo cha UDSM), Prof. Idris Mshoro (Makamu Mkuu wa Chuo cha ARU), na Prof. Burton Mwamila (Makamu Mkuu mstaafu wa Chuo cha NMIST). Naifahamu DIT kama mshindi wa mara nyingi katika masuala ya utafiti, ubunifu na teknolojia kwenye maonesho mbalimbalili ya kitaifa na

kimataifa kama vile SabaSaba (DITF). Aidha, DIT inawafanyakazi mahiri sana kwenye fani zake kwani wamezipata taaluma zao kwenye vyuo vikuu mashuhuri sehemu mbalimbali duniani. Pamoja na changamoto zinazoikabili taasisi, mimi binafsi napenda sana kujiunga na taasisi bora kama DIT ili kuipaisha Taasisi hii kufikia mafanikio ya juu sana yenye kujibu changamoto za kitaifa na hasa kulisaidia taifa letu kufikia lengo la kuwa nchi ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

**Ndugu wanafunzi,**

Leo hii nimejiandaa kuzungumzia mstakabali wa taasisi yetu katika kuandaa rasilimaliwatu (technicians and engineers) inayohitajika kwenye uchumi wa viwanda kama ilivyoazimiwa na Serikali ya awamu ya tano, inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, mkakati huu unaendana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/17 - 2020/21. DIT imebidi tujipange upya ili tuweze kuendana na matarajio mapya ya Serikali yetu na wananchi kwa ujumla.

Taasisi yetu ambayo ipo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imejipanga kuimarisha na kupanua mafunzo katika maeneo mbalimbali ya Tanzania. Naomba niwafahamishe kuwa DIT ina matawi
(kampasi) matatu yaliyopo mkoani Mwanza, Songwe (Myunga) na Dar es Salaam (Main Campus). DIT tuna lengo la kuongeza wataalam waliobobea, wabunifu na wajasiriamali ili kuongeza uzalishaji wenye tija. Pamoja na mambo mengine, mpango huu una lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 3755 hadi 6239 ifikapo 2021. Kimsingi tumeazimia kuzalisha wataalam waliobobea ambao watakuwa tayari kuanzisha na kuendesha viwanda vitakavyoanzishwa na kufufuliwa

nchini.. Lengo kuu ni kuwawezesha wahitimu wetu waweze kuajiriwa na kujiajiri bila ya kuathiriwa na ushindani katika soko la ajira.

**Ndugu wanafunzi,**

Ili kufikia azma hiyo, DIT imejipanga kuendesha mafunzo yake kiubunifu zaidi kwa kuhusisha mafunzo ya kitaalamu (technical training), teknolojia atamizi (technology incubator) na mafunzo kwa vitendo viwandani (teaching factory).

**Ndugu wanafunzi,**

Katika mkakati wa kuboresha mafunzo ya kitaalamu (technical training), DIT imejipanga kuimarisha ufundishaji wa elimu ya ufundi kwa njia mbalimbali zikiwemo kuendesha mitaala inayokidhi mahitaji ya soko na kuongeza bajeti ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kadri ya uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. Kupitia mafunzo ya karakana au maabara wanafunzi mtatakiwa kutengeneza zao halisia, kifaa au mashine zilizokamilika kwa matumizi yenu, wafanyakazi, au ya taasisi kwa ujumla. Kupitia mafunzo hayo wanafunzi mtatengeneza vitendea kazi vinavyohitajika na taasisi kama vile viti, madawati, kompyuta, magari, nk. Aidha, mkakati huu utaisaidia taasisi kuweza kumudu gharama za mafunzo kwa kutumia fedha zinazohitajika zitumike kwenye manunuzi ya vifaa vya taasisi. Badala ya taasisi kununua dhana au vifaa vya kufundishia na kujifunzia (teaching and learning materials/tools ) sasa itakuwa inanunua malighafi (mbao, misumali, gundi, nyaya, vipuli n.k.) ambazo zitachakatwa na kutengenezwa kuwa vifaa kupitia mafunzo ya darasani/maabara/karakana. Vile vile, katika mwaka huu wa fedha tutaanzisha kozi katika ngazi ya uzamili iitwayo "Sustainable Energy

Engineering," na ya mazao ya ngozi katika ngazi ya stashahada; na pia uimarishwaji wa kozi mbili za shahada za uhandisi katika mafuta na gesi, (Oil & Gas Engineering) na Teknolojia ya Mawasiliano (Information Technology).

**Ndugu wanafunzi,**

Vile vile, mafunzo kwa vitendo viwandani (Teaching factory) yatatekelezwa kwa kuanzisha viwanda vya kufundishia na/au kushirikiana na wamiliki wa viwanda halisi vya uzalishaji. Dhana ya "Teaching factory" sio ngeni sana kwani inafanana sana na ile ya "Teaching medical hospital" ambapo wanafunzi wa udaktari hufanya mazoezi ya kutibu wagonjwa halisia. Tumeshaanza kuwasiliana na wadau wa maendeleo ili watusaidie kuanzisha kiwanda cha mafunzo. Aidha, dhana hii inaweza kutekelezwa kwa kutumia viwanda ambavyo vinamilikiwa na wawekezaji baada ya kuingia mikataba maalumu ya ushirikiano. Katika mpango huu, pamoja na mambo mengine, DIT itabidi iingie mikataba na viwanda mbalimbali ili kuwawezesha wanafunzi kutembelea na kushiriki kwenye mafunzo kwa vitendo kwenye viwanda husika. Kwa kuzingatia ukweli kuwa uanzishwaji wa kiwanda au kukamilika kwa mikataba ya ushirikiano na viwanda kunaweza kuchukua muda mrefu, katika awamu hii, tumeazimia kutumia changamoto za kiufundi na kiteknolojia zinazoikabili DIT kama kiwanda chetu cha mafunzo cha kwanza. Inatarajiwa kwamba wanafunzi mtashiriki moja kwa moja katika kutatua changamoto za kiufundi zinazozikabili DIT kama vile uchakavu wa miundombinu (kupaka rangi kuta zilizochakaa; kukarabati mifumo ya maji taka, mawasiliano, umeme, n.k.). Uboreshwaji huo wa miondombinu unatarajiwa kufanywa kwa ushirikiano kati ya wanafunzi na walimu kwa kutumia tengeo la bajeti ya vifaa vya kufundishia kama

ilivyoanishwa na kuzingatiwa kwenye mpango wa manunuzi na bajeti ya Taasisi ya 2016/17. Mpango huu utaratibiwa kikamilifu ili kumpa fursa kila mwanafunzi ashiriki ipasavyo. Hata hivyo ushiriki wa mwanafunzi unaweza ukawa ni wa dharura kulingana na hali halisi ya changamoto. Katika kundi hili, changamoto za dharura ni kama vile kupasuka kwa bomba la maji au shoti ya umeme au kuzibua mifumo ya maji machafu.

Aidha, mafunzo haya yatakwenda sambamba na kutembelea na kujionea shughuli za viwandani zinavyoendeshwa katikati ya muhula wa masomo ili kuongeza uwezo wa wanafunzi katika kubuni na kutatua changamoto za kiufundi za hapa Chuoni na baadaye mara baada ya kuhitimu masomo. Hivi sasa, pamoja na kuanza kuandaa basi la Chuo tayari kwa kutekeleza mkakati huo, tunaendelea kuwasiliana na wamiliki wa viwanda mbalimbali mkoani Dar es Salaam tukiwaomba waturuhusu kutembelea viwanda vyao kwa ajili ya mafunzo ya kitaaluma.

Mnabidi kufahamu kwamba mpaka hivi sasa baadhi ya idara kama ile ya ujenzi (Civil) hasa wanafunzi wa uhandisi migodi "mining engineering" tayari wanafaidika na mpango huu wa mafunzo viwandani. Hivi karibuni pia, baadhi ya wanafunzi walishirikishwa na Taasisi kwenye miradi ya kutatua changamoto za Taasisi, wananchi na viwanda. Kwa mfano DIT ilishiriki katika mradi wa "Afya check". Mradi huu una lengo la kufanya sensa ya magonjwa yanayowasibu wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam ili Utawala wa Mkoa wa Dar es Salaam uweze kuweka mipango thabiti na endelevu ya tiba kwa waathirika. DIT ikiongozwa na Dkt. Kisanga, Dkt. Mkilania, Bw. Potini na Dkt. Msumba kwa kushirikisha na wanafunzi waliweza kutumia teknolojia ya TEHAMA kuchukua na kuhifadhi takwimu za

umati wa watanzania waliofurika kupata huduma hiyo kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja siku ya Jumamosi, tarehe 24 Septemba 2016. Wanafunzi walioshiriki katika zoezi hilo ni Grace Mathew, Bahati Tarimo, Wende Msigwa, David Stanslaus, Fredy Mwakitalima, Edward Poyongo, Henry Fanuel, Juma Ng'anzi, Godfrey Biseko, Bakari Nyerere, Abdulkarim Ramadhan, Haji Juma, Mkimbo Bernard, Michael Rogassian, Edson Nelson, na Godfrey Masau. DIT pia ikiwakilishwa na Dkt. Malisa wa Idara ya Ujenzi na Dkt. Manyele wa Idara ya "Electronics and Telecommunications" pamoja na baadhi ya wanafunzi ilishiriki katika zoezi la kutathmini madhara ya janga la tetemeko la ardhi lilitokea kule mkoani Kagera mwaka huu. DIT ilikuwa inashughulika na mambo mawili muhimu ambayo ni kutathimini ni kwa kiwango gani mihimili ya miundombinu mbalimbali iliyobaki aridhini imeathirika na nguvu ya tetemeko . Katika zoezi hili DIT ilishirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Kamati ya Maafa ya Tekemeko la Ardhi Mkoani Kagera na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera. Wanafunzi walioshiriki kwenye utafiti huo mfupi ili kuishauri Serikali jinsi gani ya kushughulikia janga lililotokea ni Katto Elisha, Alexander Alistides, Emmanuel Sombe, Muchunguzi Sospeter, na Baguma Nickson. Vilevile , DIT kupitia idara ya ujenzi inayoongozwa na Dkt. Anthony inatekeleza mradi wa upanuzi wa maabara ya upimaji udongo ikiwemo uboreshaji wa mfumo wa maji taka kwa kushirikisha wafanyakazi na wanafunzi. Wanafunzi wanaoshiriki katika mradi huo ni Grace Nzungile, Lankos Beriene, Justine Goroba, Donoth Terry, Mirahji Kheri na Selesia Msigwa.

Aidha, Taasisi hivi sasa inaboresha mfumo wa TEHAMA (OSIM) wa kudahili, kusajili, kuchakata matokeo na kuandaa vyeti ambao ulibuniwa na

kutengenezwa na mwanafunzi wa shahada ya kwanza ya Uhandisi Komptuta ambaye ni miongoni mwenu, anayeitwa Aidan Ombeni, kwa kushirikiana na mwalimu ambaye ni Hosea Shimwela. Programu hii ni mfano wa kuigwa kwani inaakisi dhana nzima ya Teaching factory ambapo wanafunzi kwa kushirikiana na walimu wanatatua changamoto za taasisi, jamii au viwanda. Kwa mantiki hiyo changamoto za DIT zimechukuliwa kama shughuli halisi za viwandani au jamii.

Kimsingi, ninapenda kusisitiza kwamba dhana ya "teaching factory" au mafunzo viwandani tayari imeshaanza kutekelezwa hapa DIT na wanafunzi niliowataja hapo awali na ambao wamesimama mbele yenu ni mashahidi na watakuwa viongozi wa mkakati huu miongoni mwenu.

Aidha, uanzishwaji wa teknolojia atamizi (**Technology incubator)** hapa DIT una lengo la kuharakisha ufikishaji na ubadilishanaji maarifa yatokanayo na utafiti na ubunifu, uliofanyika kwenye Taasisi yetu au nje kwenye soko, viwandani, au katika jamii ya kitanzania kwa matumizi. Teknolojia Atamizi inatoa nafasi, inakuza ushirikiano na ni jamvi ambalo wanafunzi watafiti, wabunifu, wajasiriamali, wanasayansi, wanateknolojia, wataalam na wawekezaji wanabadilishana maarifa, uzoefu, na wanabuni miradi na wanakuza mtandao wa ushirikiano hapa nchini, kwenye kanda yetu ya Afrika Mashariki na kote duniani.

Kimsingi uanzishwaji wa teknolojia atamizi una lengo la kuwawezesha wanafunzi wahitimu kuwa wajasiriamali ili waweze kujiajiri na kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Kwa awamu ya kwanza, dhana ya teknolojia atamizi imeshaanza kutekelezwa kwa kutumia Kampasi ya Mwanza kama

kituo cha mafunzo kwa vitendo kwa wajasiriamali (Common Facility Centre) wa mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo mikoa ya Mwanza  Shinyanga. Vile vile, wanafunzi watakaofanya vizuri katika ubunifu watapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika maonesho ya kitaifa na kimataifa. Baadhi yenu na wanafunzi wahitimu wa DIT walipata fursa ya kuonesha ubunifu wao siku ya Annual Engineers Day (1-2 Septemba 2016 iliyofanyika ukumbi wa Mlimani City) na kufunguliwa na Mhe. Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, wengine walishiriki kwenye maonesho ya wiki ya ubunifu yaliyofanyika hapa DIT kati ya tarehe 18-25 Octoba 2016 na kufunguliwa na Balozi wa Norway, Mheshimiwa Hanne-Marie Kaarstad. Hivi sasa, tunashirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na Shirika la Kimataifa lisilo la kiserikali lijulikanalo kama FESTO, kuandaa mashindano ya kimataifa ya ujuzi kwa vijana wenye umri chini ya miaka 22 yatakayofanyika kati ya tarehe 4-7 Desemba 2016. Fani zitakazoshindanishwa ni mechatronics, bricklaying and hair dressing. Tunatarajia kukaribisha wataalamu kutoka sehemu mbalimbali duniani. Nachukua fursa hii kuwaalika wanafunzi wote kujiandikisha na kushiriki katika mashindano haya kwa wingi kupitia wakuu wa idara zenu. Mashindano haya yanaratibiwa na Dkt. Utou na Dkt. Matiko. Aidha, kwa kushirikiana na taasisi  maarufu za kimataifa, DIT tunaendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali chini ya udhamini wa UNIDO, FESTO, Ushirikiano wa serikali ya India na Tanzania.

**Ndugu wanafunzi,**

Mpango huu unatambua jitihada za awali za Serikali katika mradi wa kuijengea DIT jengo la ghorofa kumi la kufundishia (Teaching Tower

Complex) ambalo linatarajiwa kuongeza udahili wa wanafunzi wapatao 984 punde litakapokamilika mwaka huu wa masomo. Vile vile, DIT kwa kutambua umuhimu wa wahitimu wa DIT katika kutuwezesha kufikia malengo haya, tumeshaanzisha mawasiliano ya karibu na Alumni kwa kupitia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii na tovuti ya Taasisi. Mpaka hivi sasa tuna mtandao wa Alumni wapatao zaidi ya 400 ambao wameahidi kutusaidia katika nyanja mbalimbali ikiwemo kututafutia sehemu za kufanyia mafunzo viwandani mwisho wa mwaka (IPT) na kuja kuendesha mihadhara ya kitaaluma kwa wanafunzi na wafanyakazi. Mhadhara wa kwanza utafanyika siku ya Jumatano, tarehe 16 Novemba 2016 kwenye Ukumbi wa Bunge hapa Dar es Salaam, ambapo Wahitimu Mashuhuri wawili wa DIT, Prof. Mathew Luhanga na Prof. Burton Mwamila; watakuja kuendesha mhadhara unaohusu uongozi katika taasisi za elimu ya juu kwa viongozi wa Chuo. Tunatarajia kuandaa mihadhara ya namna hiyo na hasa ile ya kuwaandaeni kujiajiri kadri ya ratiba ya masomo (Almanac) itakavyoruhusu.

**Ndugu wanafunzi,**

Kwa kuzingatia muktadha huo, uongozi wa DIT unakuomba wewe kama mwanafunzi, Alumni mtarajiwa na mdau katika maendeleo ya Taasisi:

- Ushiriki kikamilifu katika mpango huu wa uboreshaji wa taaluma ya ufundi hapa DIT.
- Kutumia kwa uangalifu na kulinda miundombinu ya taasisi ili tuweze kuyafikia malengo yetu ya kuboresha taaluma ya ufundi.
- Uwe tayari kutumia muda wako vizuri na hata wa ziada ili kuweza kutatua changamoto zinazoikabili taasisi yetu kama vile kutengeneza bidhaa na vifaa bora na kamilifu kupitia mafunzo ya darasani.

Tunatarajia wanafunzi mtashiriki moja kwa moja katika kutengeneza viti kwa ajili ya kukalia madarasani, ofisini; mtapaka rangi kuta zilizochakaa; mtafanya service ya magari ya taasisi, mtakarabati mifumo ya simu na umeme, kompyuta, n.k.

- Mtajitolea kwa hali na mali pale mtakapohitajika kutatua changamoto za jamii kama vile majanga na dharura mbalimbali.
- Mtatumia fursa ya mafunzo ya viwandani katikati ya muhula kikamilifu kwa manufaa ya taasisi na yenu binafsi baada ya kuhitimu mafunzo.
- Mtaanza kushirikiana na walimu na wafanyakazi katika kuanzisha na kuendeleza mawazo yenu binafsi ya uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo au vya kati kabla hamjahitimu masomo.
- Wanafunzi watakaofanya vizuri katika ubunifu na ujuzi wawe tayari kushiriki katika maonesho na mashindano mbalimbali ili kukuza vipaji na kujitangaza kwa wawekezaji.
- Mtaanza kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo na Alumni katika kukuza mawazo yenu ya kujiajiri mapema kabla ya kuhitimu masomo.
- Mtazingatia nidhamu wakati wote mtakapokuwa hapa Chuoni na kama mtapatwa na changamoto yoyote mnaombwa mfuate taratibu zilizowekwa. Ni matumaini yenu mtakuwa mnatumia Baraza la wanafunzi kwa ufanisi zaidi kwa kujadili hoja mbalimbali kabla hazijafikishwa kwenye uogozi wa Chuo kwa utekelezaji.
- Ili kufanikisha azma hii na makusudio ya mpango huu, afya njema kwa wanafunzi ni muhimu. Kwa hiyo tunawashauri wanafunzi wote mjali na mlinde afya zenu kwa kuepuka magonjwa yanayoambukiza (AIDS na TB). Kama nilivyowashauri wale wa mwaka wa kwanza

mjitahidi kujiamini kwamba mnaweza kuvishinda vishawishi (wadada warembo na wakaka bomba). Belive in yourself and stay safe!

**Ndugu wanafunzi,**

Pamoja na kueleweka kwa hoja ninazozitoa kwenye hotuba yangu nadhani bado baadhi yenu, hasa wale waliokaa hapa Chuoni muda mrefu, wanajiuliza haya mambo yanawezekana vipi ukizingatia kuna changamoto lukuki katika kuendesha Chuo?

Ukweli ni kwamba Uongozi wa Chuo na wafanyakazi wote kwa pamoja wanazifahamu hizo changamoto hasa zile zinazowakabili wanafunzi. Hata hivyo wafanyakazi wameshakubaliana kupambana na changamoto hizo kwa hali na mali. Mambo ambayo tunayafanyia kazi ni pamoja na kutoshirikishwa kikamilifu kwa wanafunzi katika maamuzi ya taasisi; upungufu wa vifaa vya kufundishia, uchache na uchakavu wa miundombinu kama vile mabweni/madarasa/maabara/karakana, ucheleweshwaji wa matokeo ya mitihani na vyeti vya kuhitimu, ufinyu wa nafasi za mafunzo ya viwandani na ushindani katika soko la ajira.

**Ndugu wanafunzi,**

Labda niseme kuwa, hotuba ya leo, pamoja na mambo mengine, imejikita kutatua changamoto ya kwanza kabisa ya kutoshirikishwa kikamilifu kwa wanafunzi katika mikakati muhimu ya taasisi. Kimsingi, labda niseme kwamba hotuba nilizotoa tarehe 4 Novemba 2016 kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na hii ya leo tarehe 11 Novemba 2016 kwa wanafunzi wote na zingine zitakazokuja hapo baadaye zimejikita katika kushirikisha wanafunzi kama wadau wakubwa kwenye mambo muhimu ya taasisi. Leo

hii vile vile, baada ya hotuba yangu, mtapata fursa ya kuuliza maswali na kuchangia mawazo yenu katika kuboresha dhana ya "Teaching factory" na maendeleo ya taasisi yetu kwa ujumla.

Aidha, changamoto za upungufu wa vifaa vya kufundishia, uchache na uchakavu wa mabweni/madarasa/maabara/karakana, ufinyu wa nafasi za mafunzo ya viwandani na ushindani katika soko la ajira zinajibiwa moja kwa moja na dhana ya "Teaching factory" kama nilivyosisitiza hapo awali kwenye hotuba yangu.

Katika kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa matokeo ya mitihani na vyeti vya kuhitimu kuanzia mwaka huu wa masomo taasisi imeanza kutumia mfumo bora zaidi wa TEHAMA katika kuchakata matokeo ya mitihani na kuandaa academic transcripts (nakala ya kielimu). Aidha, taasisi imeandaa ratiba maalum ya shughuli zote za taaluma na utawala iitwayo Almanac ambayo inabidi izingatiwe na kila mwanachuo yaani wanafunzi na wafanyakazi katika utendaji wao wa kazi. Unaweza kuisoma Almanac kwenye tovuti ya Chuo (www.dit.ac.tz). Tunaamini kuwa kwa kuzingatia Almanac hakutakuwa na ucheleweshwaji wa matokeo au vyeti bila sababu maalum. Vilevile wafanyakazi wote tumekubaliana kuboresha utoaji wa huduma zetu zote kwa wateja wetu wakiwemo wanafunzi. Tumeshaweka mifumo stahiki ya kisasa na ya kisheria ya kujipima katika utendaji wetu wa kazi.

**Ndugu wanafunzi,**

Katika kumalizia hotuba yangu, nawashauri mtumie muda wenu kuwasiliana na washauri wa kitaaluma (academic advisors) mara kwa mara

ili mpate ushauri stahiki kwa wakati; hii itawasaidia kuepuka matatizo ya kitaaluma yanayoweza kujitokeza. Mwisho kabisa napenda niwashukuruni kwa kunisikiliza kwa makini na nakaribisha mapendekezo na maswali kama yapo.

**Asanteni sana!**